JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI NYAILIGAMBA,
S.L.P 1523,
BUKOBA.

NDUGU……
S.L.P ……
……..

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI NYAILIGAMBA HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA MKOA KAGERA MWAKA WA MASOMO 2022/2023.

Jumuiya ya wafanyakazi wa shule ya sekondari **Nyailigamba** , wanafunzi pamoja na mimi binafsi tunafurahi na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha **TANO** kwa mchepuo wa PCM/CBG/HGL,/HGK,/ HKL katika shule hii. **HONGERA NA KARIBU SANA**.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo mkoa wa Kagera Wilaya ya Muleba umbali wa km 40 tu kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Muleba barabara iendayo Bukoba mjini kituo cha Magari Muhutwe na barabara inayoenda kamachumu Km 1 kutoka kwenye rami barabara iendayo Kamachumu utaona kibao cha Shule . Kwa wale wanaotoka Bukoba mjini kwenda Muleba wateremkie Muhutwe na wale wanaotoka nje ya mkoa wa Kagera kupitia barabara ya Biharamlo kuelekea bukoba mjini wateremkie kituo cha magari Muhutwe. Kutoka Muhutwe stendi utaelekea barabara ya kamachumu Km 1 kutoka hapo kwa kutumia bodaboda. Nauli ya bodaboda ni shilingi mia tano hadi elfu moja tu. Shule inayo miundo mbinu ya Umeme pamoja na Maji.

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE.

Kwa kuzingatia azima ya sera ya Elimu ya kuwahamasisha wazazi kuchangia gharama za uendeshaji wa elimu katika shule za serikali mwanafunzi ili aweze kupokelewa shuleni hapa, anatakiwa kulipa gharama zifuatazo:-

A: (i)**KARO**

Unatakiwa kulipa karo ya shule Tsh. 70,000/= kwa mwaka, au unaweza kulipa Tsh.35,000/= kwa Muhula. Karo iwekwe kwenye **A/C Na.32001200059** jina la akaunt **ni MDC NYAILIGAMBA SECONDARY SCHOOL** katika benki ya **NMB** tawi lolote liliko karibu na wewe.

Pamoja na karo kuna michango inayotakiwa kulipwa katika benki nayo ni.

1. Mchango kwa ajili ya ukarabati wa samani Tsh. 15,000/= (**Inalipwa mara moja**)
2. Pesa ya taaluma Tsh. 20,000/= **kwa mwaka** au 10,000/= (**kila muhula**)
3. Pesa ya matibabu Tsh. 20,000**/= kwa mwaka.**
4. Pesa ya mlinzi,wapishi pamoja na vibarua wengine Tsh 30,000/= (**Inalipwa kila mwaka**)
5. Tsh. 5,000/= ,Pesa ya tahadhari **(haitarejeshwa**)
6. Tsh. 6,000/= kwa ajili picha na kitambulisho **(Inalipwa mara moja**)
7. Tsh. 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule (**inalipwa mara moja**]
8. Tsh 20,000/= kwa ajili ya Mitihani.

Angalizo

 Mwanafunzi atalipa jumla ya ada na michango kwa Mwaka Tsh. **188,000/=**

B) MAHITAJI YA KUJANAYO SHULENI.

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo:-

1. Jembe 1 na mpini ,Dekio(squeezer/drier) yenye mpini wake, kwa ajili ya usafi.

 Fyekeo na reki kwa ajili ya usafi.

2. Ndoo, 1 ya plastic ya lita 20. 1 na beseni 1 ya kuogea na kifaa cha lita mbili
Kwa ajili ya kuhifadhia maji safi ya kunywa.
3 Vifaa vya kulia chakula: bakuli ,sahani, kikombe na kijiko pamoja na vifaa vya usafi binafsi mf: mswaki, dawa ya meno kubwa, dawa ya viatu kubwa, mafuta ya kujipaka kopo kubwa, sabuni za kufua na kuoga, kanda mbili/yebo taulo, kwa wasichana: pea moja ya kitenge, na vifaa kwa ajili ya usafi wakimaumbile.
4.Ream 1 ya karatasi za A4 (Italetwa kila MUHULA)
5.Kokotoo la hesabu (Scientific Calculator) kwa wanaosoma Hesabu.
6.Mathematical set kwa wale wanaosoma geografia na hesabu
7.Godoro lenye urefu futi 6 upana futi 2 ½.
8.Mwanafunzi atatakiwa kuwasilisha bahasha na stamp kila muhula kwa ajili ya kutuma taarifa za mitihani.
9.Chandarua moja ya pembe nne.
10.Mwanafunzi aje na kadi ya bima ya afya kwa ajili ya huduma za hospitali. NA ambaye hana Bima aje na Tsh 54000/= KWA AJILI YA KUKATIWA BIMA YA AFYA (NHF) (FEDHA YA BIMA ILETWE SHULENI)
11.Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma somo la **BIOLOJIA**

a) **SARE YA SHULE**.
Unatakiwa kuwa na mavazi yafuatayo;-
1. Sketi mbili nyeusi za marinda ya kuelekea upande mmoja upana wa marinda ni inchi mbili (**Knife edge**) Upana wa mkanda usizidi inchi mbili. Urefu wa sketi kutoka kwenye magoti iwe inchi sita chini ya magoti, kitambaa kizito).
2. Shati mbili nyeupe mikono mirefu aina ya Tetron, lenye vishikizo vya kawaida na mfuko mmoja upande wa kushoto.
3. Jozi 2 za viatu vyeusi vya ngozi visiwe buti. Viatu visiwe na madoido viwe na visigino vifupi na vyenye kufungwa kwa kamba
4. Soksi nyeupe jozi mbili.
5. Tai nyeusi.
6. Sweta yenye nembo ya shule inapatikana karibu na shule.
7. T-shirt 2 zenye nembo ya shule zinapatikana karibu na shuleni.
8. Kamusi ya Kiingereza kwa kiingereza (**Advanced Dictionary**)
9. Madaftari makubwa (**Counter Books** 7)
10. Kalamu za wino za kutosha.
11. Njoo na shuka jozi mbili, blanketi moja na mto mmoja (Mashuka yawe **rangi ya pinki** na yawekewe alama kuondoa usumbufu wa kupotea).
13. **Kwa wanafunzi wa kiislamu** watatakiwa kuwa na sketi nyeusi ndefu mbili zenye malinda jarabibi nyeupe na panjabi mbili nyeupe zenye urefu sawa na shati. Kwa shughuli za nje atatakiwa kuja na sketi mbili ndefu za rangi ya zambarau pamoja na jarabibi na Panjabi za rangi nyekundu.
14. Wakati wa shughuli za nje baada ya saa za masomo kama vile shughuli ya usafi,uzalishaji na michezo unatakiwa kuvaa skirt rangi ya zambarau na T-shirt yenye nembo ya shule.
Hivyo utatakiwa **kuja na sketi mbili za rangi ya zambalau zenye mshono wa heshima kitambaa kizito**
15. Kamusi ya Kiingereza. [Advanced learners DICTIONARY]
16. Vitabu vyaTahasusi husika; ADVANCED BIOLOGY, UNDERSTANDING BIOLOGY, BIOLOGICAL SCIENCE, FUNDERMENTAL APPROACH, PRINCIPAL OF CLASSIFICATION, RAMSDEN CHAND, PRINCIPLES OF PHYSICS BY NELICON, PRINCIPALS OF PHYSICS BY CHAND (CLASS XI AND CLASS XII), RONGER MUNCASTER, WORKED EXAMPLES IN A-LEVEL PHYSICS AND MATHEMATICS BY CHAND. Kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sanaa mnashauliwa kuwa na vitabu vinavyoendana na Tahasusi yako.

17. T-Shirt ya michezo **aje nayo nyekundu na bukta ya blue**.
18. Kwa ajili ya baridi na mbu wakati wa usiku utavaa track suit rangi nyekundu hivyi ni lazima uje na **Track suit**

C

i) Nywele fupi zisizozidi sentimeta moja na si vinginevyo.
ii) Hairuhusiwi kubadili ngozi (**kujichubu**a) **KUTOKANA NA MATATIZO MBALIMBALI YA KIAFYA YA WANAFUNZI, KAMWE MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUTUMIA PAFYUMU**
iii) Rangi kwenye kucha, wanja, na urembo mwingine kwa wasichana ni marufuku.
vii) Aje na viatu vya michezo (**Raba nyeupe**).

NB: Kwa kuwa tunategemea mwanafunzi atavaa sare ya shule kila wakati, nguo nyingine tofauti na sare tajwa,HAZIHITAJIKI. Kwa wanaotoka mbali wasiliana na uongozi wa shule ili kujua baadhi ya vifaa vinavyopatikana katika Mazingira yaliyokaribu na Shule ili kuondoa usumbufu katika safari.

MAMBO YAKUZINGATIA

a) Nidhamu ni msingi wa **MAFANIKIO**

b) Fomu za kurudisha shuleni ni pamoja na:-

1. Kauli ya kukubali **(KK)**
2. Mahusiano na malezi (**MM)**
3. Request for medical examination
4. Hati ya uraia au Birth Certificate.

 Usajili utafanyika baada ya kukamilisha maelekezo yote
 Muhula wa Masomo utaanza KAMA ITAKAVYOELEKEZWA NA MAMLAKA HUSIKA.
Unashauriwa kufanya mawasiliano
kwa ajili ya kufahamu kama kuna mabadiliko ya tarehe ya kuripoti au kama utahitaji ufafanuzi zaidi.
 Mwanafunzi Haruhusiwi Kuja Na Simu Ya Mkononi Shuleni, Akipatikana Nayo Atafukuzwa Shule.
 Iwapo kuna tatitizo lolote mawasiliano yoyote juu ya mwanao yafanyike kupitia namba zifuatazo:-

0764760360 (**Mkuu wa shule**)
0684543984(**Makamu mkuu wa shule**)
0769526863 (**Mwalimu wa nidhamu**)
0763838208 (**Mwalimu wa taaluma**)

Kumbuka, maelezo yote ni muhimu, usajili utafanyika baada ya kukamilisha Mahitaji.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYAILIGAMBA
MWENYEZI MUNGU AKUTANGULIE KATIKA SAFARI YAKO.

.....
A. A. KASHAMBA.
MKUU WA SHULE.

KAULI YA KUKUBALI (KK)
SHERIA ZA SHULE

Wakati wowote watu wanapoishi na kufanya kazi pamoja huwa hapana budi sheria na kanuni ziwekwe ili kurahisisha uhusiano mwema katika mwenendo wa wale wanaohusika. Sheria zifuatazo zimewekwa ili kusaidia mwanafunzi kujiepusha na mambo ambayo yanaweza kusababisha asihitimu masomo yake.

Sheria hizi ni nyongeza tu kwa zile ambazo ni sheria za nchi na mila zetu na ambazo kila mzalendo anapaswa kuzifuata.

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika mahudhurio ya kila siku hapa shuleni kama vile masomo, mikutano, kazi za kuzalisha mali, michezo na shughuli nyinginezo zitakazoandaliwa na shule.
2. Kila mwanafunzi atavaa nguo rasmi za shule wakati wote awapo shuleni. Nguo hizo zishonwe kwa mtindo wa heshima ulioamuliwa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi.
3. Kila mwanafunzi atatakiwa kujiheshimu mwenyewe na kuheshimu watu wote hapa shuleni nan je ya shule. Atatakiwa kuonesha adabu kwa wnaomzidi umri na awe na utii na ushirikiano kwa walimu, wafanyakazi na serikali ya wanafunzi.
4. Kila mwanafunzi atakuwa na wajibu wa kulinda na kuhifadhi mali ya umma isiharibike kwa makusudi hana budi kulipa gharama.
5. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutembelea nyumba za starehe, vilabu vya pombe au baa pamoja na nyumba za wafanyakazi isipokuwa kwa kibali maalumu.
6. Mwanfunzi atakayejihusisha na ulevi na pombe madawa ya kulevya, na uvutaji sigara au bangi hatakuwa mwanafunzi wa shule hii. Hii ina maana hata wakati wa likizo.
7. Utoro au uzururaji wakati wa masomo au wakati wa kazi asa uzalishaji mali ni marufuku. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kukaa katika mazingira ya shule wakati wote wa masomo, hata baada ya masomo isipokuwa kwa kibali maalumu.
8. Mwanafunzi wa kike akipatikana na mimba ataondolewa shuleni mara moja. Ikithibitika kuwa mwanafunzi wa kiume amempa mimba mwanafunzi pia ataondolewa shuleni.
9. Wizi wa aina yoyote ni marufuku kabisa na yeyote atakayeshiriki tabia hii mbaya ataondolewa shuleni mara moja mbali na kuandamwa na sheria za nchi.
10. Lugha inayotumika shuleni ni kiingereza akibainika mwanafunzi anatumia lugha tofauti na hiyo ataadhibiwa.
11. Kila mwanafunzi atashiriki katika shughuli za uzalishaji mali ka vile kilimo pamoja na usafi wa mazingira kwa mujibu wa ratiba. Kutoshiriki kwa makusudi kwa kutumia visingizio/ujanja wa aina mbalimbali hautakubalika.

12. **Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii. Ukikamatwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa / kibali utarudishwa nyumbani na wakati unarudishwa shule utatakiwa kuwa na waya wa uzio (fense wire) yenye thamani ya Tsh. 120,000/=**
13. **Huruhusiwi kumiliki simu shuleni na endapo utabainika utasimamishwa masomo na kulipa faini ya kununua umeme wenye dhamani ya Laki moja (100,000/=).**

.Makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi **KUFUKUZWA** shule ni :

i) Wizi

ii) Usherati, ubakaji na ushoga

iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

iv) Uvutaji wa bangi na sigara

v) Makosa ya jinai

vi) Kupiga au kupigana

vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

viii) Kudharau bendera ya taifa

ix) Kuoa au kuolewa

x) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule

xi) Kutoa mimba

xii) Kugoma kuchochea na kuongoza au kuvunja amani na usalama wa watu /shule.

xiii) Utoro uliokithiri

xiv) Kukataa adhabu kwa makusudi

xv) Kumiliki simu shuleni(Mawasiliano yote yafanyike kupitia uongozi washule kwa namba zilizotajwa)na sikumpa mwanafunzi simu hatutampokea kwa sababu yoyote**.**

NB: Hakikisha wakati wote unatenda mambo ambayo hayatamfanya mwalimu /kiongozi kuhisi kuwa umevunja au unataka kuvunja taratibu za shule kwa kufanya hivyo utafukuzwa shule. Mambo yote yaliyotajwa hapo juu yanatakiwa kuzingatiwa ili mwanafunzi aweze kumaliza shule salama.

Mwanafunzi anatakiwa kujijengea au kusaidiwa kujenga Nidhamu ya dhati ili aweze kufanikiwa maishani. Mwanafunzi mwenye nidhamu bora ni Yule anayeheshimu wazazi na walimu wake,mafanikio yake yanategemea nguzo hizi mbili, ni lazima awe na Nidhamu ya dhati shuleni kwa maisha ya baadae.

Mwanafunzi asipewe simu kwa kisingizio cha kuitumia awapo safarini maana vyombo vyote vya usafiri atakavyotumia watakuwemo abiria wenye busara watakaomsaidia mawasiliano mara apatapo shida.

AHADI YA MWANFUNZI KWA UONGOZI WA SHULE

Nimezisoma Sheria /Kanuni hizi na kuzielewa nitazitimiza .

Jina la Mwanafunzi……

Sahihi ya Mwanafunzi……..

Jina la Mzazi/ Mlezi ……..

Tarehe ……..

IJAZWE NA MZAZI/MLEZINA KURUDISHWA SHULENI

ANWANI YA MLEZI
……..
……..
TAREHE……

KUMB NA……..
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NYAILIGAMBA
S.L.P. 1523,
MULEBA.

YAH: MALEZI YA MTOTO ……KIDATO CHA……MWAKA……

NIMEZISOMA SHERIA NA Kanuni za shule Kumb.Na.NYB/SS/01 na kuzielewa.
Ninapenda kuhakikisha kwamba mimi mzazi/mlezi wa mtoto huyo /niko tayari kusaidiana na shule katika jitihada zote za kumjengea mtoto wangu nidhamu ya dhati.
Naahidi nitajitahidi kumwongoza kwenye masomo yake kulingana na taratibu za shule.
ZINGATIA:
i. Asikose kuhudhuria shuleni kama hakuna sababu ya msingi ya kumzuia na akikosa, apewe kibali toka kwa mzazi/mlezi wake bila hivyo hatapokelewa.
ii. Asijihusishe na matendo ya utoro , uzururaji, matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vinginevyo ambavyo vinaweza kumzuia kuendelea na shule.
iii. Asipuuze au kukataa kuhudhuria miradi ya shule , kama vile kilimo na kutunza usafi wa mazingira.
iv. Asijihusishe na migomo au ushawishi wowote unaoweza kuvunja amani ya shule kwani kwa kufanya hivyo atafukuzwa shule mara moja.
v. Akazanie masomo kwa lengo la kufaulu mitihani yake ya ndani nayanje .

…… ……
JINA KAMILI MZAZI/MLEZI SAHIHI

MEDICAL EXAMINATION FORM DATE……NAME OF

STUDENT……

To medical office I/C of …….. District/Regional;/Referral/Designated

Hospital : P.O.BOX ……..

Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for

Being able to pursue years of University Studies. In case of an acute

defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible

of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

Eye sight……..

Heart examination ……

Blood pressure ……..

Hearing ……..

Speech ……

Venereal Disease ……

Leprosy ……

Epilepsy ……

Stool routine ……..

Urine routine ……

Sickle cell test ……

OBP including: ESR…….. B/S……..

HB……

Others……...

Name……..Signature……...

DESIGNATION……
OFFICIAL STAMP……..
DATE……

.ANGALIZO:Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na sahihi ya mganga .Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukuwa vipimo sahihi atarudishwa nyumbani.